

## Coronavirus (COVID-19)

# Upimaji wa COVID-19

## Kwa nini nipimwe?

Yeyote ambaye ana dalili ZOZOTE za mafua au kama homa ya mafua, hata kama ni KIDOGO, anapaswa kupata kipimo cha COVID-19, haraka iwezekanavyo. Dalili za COVID-19 ni pamoja na:

- homa k.m. baridi, jasho ya usiku.
- dalili za kupumua kama vile kikohozi, koo yenye maumivu/kukuna,kamasi nyingi puan, upungufu wa pumzi, kupoteza hisia za harufu au ladha.
- dalili zingine ikiwa pamoja na maumivu ya misuli na viungo, kuhararisha, kichefuchefu/kutapika na kupoteza hamu ya kula.

## Nini cha kutarajia unapopimwa?

- Upimaji ni bure, rahisi na upesi.
- Ikiwa umeelekezwa kwa kliniki ya upimaji, tafadhali chukua barua ya kuelekeza nawe.
- Wafanyakazi katika kliniki za upimaji na magonjwa ya kupumua watakuwa wamevaa vinyago (masks), gauni, glavu na kinga za uso.
- Swabs huchukuliwa na kifaa cha nyembamba ya pamba kutoka ndani ya pua na koo yako.

## Nini inatokea baada ya nimepimwa?

- Unapaswa kukaa nyumbani (kujitenga) hadi upate majibu yako ya kipimo na uko mzima.
- Huwezi kuondoka nyumbani kwako isipokuwa unatafuta huduma ya matibabu au dharura. Huwezi kuwa na wageni.
- Ikiwa dalili zako zinakuwa kubwa (k.m. ugumu wa kupumua), pigia simu Sufuri Tatu (000). Waambie wafanyakazi wa ambulensi kuwa umepimwa kwa COVID-19.
- Ikiwa unashiriki nyumba yako na wengine unapaswa kujitenga katika chumba kingine. Vaa mask ya upasuaji wakati uko katika chumba kimoja na wengine na uweke umbali wa mita 1.5.
- Fanya usafi mzuri. Osha mikono yako mara nyingi. Funika kikohozi chako na kupiga chafya kwa kutumia kiwiko chako au tishu.

## Naishi na mtu anayehitaji kujitenga. Je! Nawea kupata wapi habari zaidi juu ya kujitenga?

<https://www.health.nsw.gov.au/Infectious/covid-19/Pages/resources.aspx>

- Ikiwa umekuwa ukiwasiliana sana na mtu ambaye ana COVID-19, unahitaji kukaa nyumbani kwa siku 14 baada ya kumuona mtu huyo mara ya mwisho. (Kuwasiliana kwa karibu ni pamoja na kuishi katika kaya moja au kushinda zaidi ya dakika 15 kwa uso kwa uso au masaa 2 kushiriki nafasi iliyofungwa, na mtu aliye na COVID-19, kuanzia muda wa masaa 48 kabla ya aliugua).
- Kutengwa nyumbani kunatumika kwa mawasiliano wote wa karibu, hata ikiwa kwa sasa unajisikia vizuri na au umepokea majibu ya kipimo kwamba huna.

## Nitapata majibu jinsi gani?

- Kawaida utapokea majibu yako ya kipimo katika masaa 24 hadi 48 lakini tafadhali tarajia hata hadi masaa 72.
- Ikiwa kipimo chako kilifanywa katika Idara ya Dharura au kliniki ya COVID-19 ya hospitali ya umma unaweza kupokea majibu yako kuwa huna COVID-19 kwa njia ya SMS ikiwa umejiandikisha kwa Pathology COVID-19 SMS Results Service (Huduma ya Majibu ya Ujumbe SMS wa COVID-19 ya Patholojia). Ukikosa kuijiandikisha utapokea simu kutoka kwa afisa wa Afya ya Umma kutoka Wilaya ya Afya ya Mitaa.
- Ikiwa kipimo chako umekusanya na GP/daktari wako au kwenye eneo lingine, daktari wako atakupa majibu yako.

## Nini inatokea ikiwa napimwa kuwa navyo?

- NSW Health itakutunza. Hakuna malipo kwa tiba yako, hata ikiwa huna Medicare.



# COVID-19 Testing

## Naweza kupimwa wapi?

- Tembelea kliniki ya COVID-19:  
<https://www.health.nsw.gov.au/Infectious/covid-19/Pages/clinics.aspx>  
AU
  - Piga simu daktari yako

## **NSW Health COVID-19 testing clinic locations:**

## Mahali pa kliniki ya kupima ya NSW Health COVID-19: